

## **Wafanyabiashara Ruvuma wanavyonufaika na mikopo kupitia NMB BUSINESS CLUBS**

MIIKOPO inayotolewa na Benki ya NMB hapa nchini, kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati wa NMB Business Club imefikia thamani ya shilingi bilioni 600 .

Akizungumza katika warsha ya NMB Business Club mkoani Ruvuma ambayo imefanyika kwenye ukumbi wa Heritage mjini Songea Meneja Mwandamizi Idara ya Biashara kutoka NMB Makao Makuu Wogofya Mfalamagoha anasema NMB Business Club imelenga kuwafikia jamii ya wafanyabiashara wadogo na wafanyabiashara wa kati ambao ni zaidi ya 200,000 nchi nzima.

Mfalamagoha anasema NMB Business Club ni mahali sahihi pa kuelimisha wafanyabiashara kuhusu masuala mbalimbali ya biashara zao na kwamba katika nchi nzima kuna jumla ya Business Club 36 ambapo kila mmoja ina wanachama kati ya 150 hadi 300 ambao wamekuwa wanafaidika na mafunzo mbalimbali kutoka NMB.

“Lengo ni kuhakikisha ninyi wafanyabiashara mnakuza mitaji yenu, kuajiri watazania wengi zaidi na kuchangia uchumi wa Taifa kwa kupitia ulipaji kodi”, anasisitiza Mfalamagoha.

Kulingana na Meneja huyo, wafanyabiashara wadogo na wakati wanawakilisha asilimia 17 ya biashara yote ya NMB na kwamba ni jambo la kujivunia kuona tabaka hilo la wafanyabiashara wanakua kwa kasi ya kuridhisha na NMB.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa NMB Business Club mkoani Ruvuma Abraham John, anayataja mafanikio ambayo

yamepatikana kwa wafanyabiashara wa NMB kupitia Klabu hiyo kuwa ni kupewa elimu ya biashara,masoko,kukuza mtaji na kutoa elimu ya ulipaji wa kodi na leseni.

Mafanikio mengine anayataja kuwa ni NMB imeweza kupunguza muda wa kupata mkopo,kuongezewa maeneo ya kukaa wateja,kuongezwa mashine za ATM,kutengeneza sehemu ya maliwato ya wateja na ongezeko la muda wa huduma za kibenki toka saa 9.30 hadi saa 10.30 tofauti ya Benki nyingine.

“Tunawapongeza NMB mkoani Ruvuma kwa sababu wameweza kuondoa masharti ya kuwa na akaunti ya mkopo,ongezeko la Taller,ongezeko la kiwango cha mkopo unaotolewa kwenye tawi toka milioni 15 hadi milioni 50 hivi sasa na ongezeko la muda wa marejesho kutoka mwaka mmoja hadi zaidi ya mwaka mmoja”,anasema.

Mwenyekiti huyo anashauri kuwe na uongozi wa Klabu katika kila tawi la NMB ili wawe na fursa ya kujadili mambo na kutafuta suluhisho la kutatua changamoto za wadau katika tawi husika.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Meneja wa NMB Kanda ya Kusini Goodluck Shirima anawashukuru wafanyabiashara hao kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wanautoa katika matawi yote ya NMB katika Kanda ya Kusini.

Hata hivyo Meneja huyo anawakumbusha wafanyabiashara hao kuhusu mikopo ambayo walikuwa wanaitumia na elimu ambayo wamekuwa wanaitoa kwa miaka nane iliyopita na kwamba hivi sasa Benki ya NMB itakuwa katika utendaji kutoka kutoa mikopo kwa wazazi na Kampuni hadi kutoa huduma za kifedha katika ngazi ya familia.

“Wasiwe tu wazazi au Kampuni ndiyo inafanya shughuli za kibenki na NMB,badala yake sasa familia yote wakiwemo watoto wadogo wawe wateja wetu wa Benki ya NMB,habaki mtu tunasonga mbele pamoja”,anasisitiza.

Ili kufanikisha hilo Meneja huyo wa Kanda anasema hivi sasa NMB inatoa elimu ya masuala ya kifedha katika shule za msingi na sekondari ili waweze kufaidika na Benki ya NMB.

Wilfred Lukumay ni Meneja Huduma za Wakala Kanda ya Kusini anasema kuna kuna idadi kubwa ya wafanyabiashara wa NMB Bussines Club kutoka mkoani Ruvuma ambao wameunga mkono katika biashara ya wakala wa NMB.

Hata hivyo anabainisha kuwa hivi sasa NMB imesitisha kwa muda huduma za Wakala wa NMB ili kufanya maboresho kwa kuingiza Kampuni nyingi zaidi ikiwemo maji na huduma za hospitali,umeme na kufanya uboreshaji wa mifumo ya teknolojia kabla ya kuanza tena huduma za mawakala.

Naye Glory Kimaro ambaye ni Meneja Uhusiano Kitengo cha Biashara NMB Makao Makuu,anasema NMB ina kitengo ambacho kinashughulikia mikopo mikubwa inayoanzia milioni 100 hadi bilioni 2.5 hivyo amewashauri wafanyabiashara wa Mkoa wa Ruvuma kutumia kitengo hicho ili kukuza uchumi wao na kuchangia pato la Taifa.

Katika warsha hiyo wafanyabiashara wadogo wa NMB Business Club mkoani Ruvuma wametoa ushuhuda wao namna walivyofanikiwa kupitia NMB ambao hivi sasa wanamiliki mitaji mikubwa na kuendelea kunufaika na mikopo kupitia NMB.

Albano Ngovano ni Mfanyabiashara wa mjini Songea ambaye alianza biashara kwa kukopa shilingi 150,000 mwaka 2003 ambapo hivi sasa kupitia Benki ya NMB anakopeshwa hadi milioni 150.

Kupitia mikopo hiyo Ngovano anasema ameweza kupata maendeleo ikiwemo kumiliki duka la vifaa na bidhaa za jumla,amejenga nyumba kadhaa na kumiliki magari matatu .

“Nawashukuru sana NMB kwa kweli bila wao maendeleo niliyoyapata yasingekuwepo,ningekuwa bado katika maisha ya umasikini,NMB wamekuwa jirani na mimi kwa kunisikiliza na kunipa elimu ya biashara”,anasema Ngovano.

Naye Ashers Bhatia Mfanyabiashara kutoka wilayani Namtumbo anasema NMB imemwezesha kuunganisha familia yake kibiashara ambapo mtoto wake wa kike mwenye umri wa miaka 20,ambapo Oktoba 2018 aliweza kukopeshwa na NMB shilingi milioni 10 ambaye alitakiwa kurejesha katika kipindi cha miezi tisa ambapo Agosti mwaka huu anamaliza mkopo huo.

“Familia kuwa na biashara inasaidia kupunguza migogoro katika familia,kwa sababu kila mmoja anamudu kuendesha maisha yake na kuacha tabia ya kuwa tegemezi kwa wazazi,hata ukifa unamwacha mtoto wake anaendesha maisha bila wasiwasi”,anasisitiza.

Chama cha Ushirika wilayani Songea na Namtumbo (SONAMC) kimekuwa kinadaiwa na NMB mkopo wa zaidi ya shilingi bilioni mbili na kwamba licha ya deni hilo NMB katika msimu wa mwaka 2017/2018 ilikubali kutoa mkopo mwingine kwa chama hicho

baada ya chama hicho kupata masoko ya zao la tumbaku kwa wakulima.

Mwakilishi wa SONAMC Zamakanaly Komba akitoa ushuhuda namna chama hicho kilivyosaidiwa na NMB anabainisha kuwa iliwalazimu kukopo tena NMB licha ya kuwa na deni na kwamba NMB walikubali kukikopesha chama hicho bilioni 1.177.

“NMB ni Benki ambayo inasikiliza shida za wateja wake,tumeenda nao vizuri ambapo tumeweza kulipa mkopo za zaidi ya bilioni moja ndani ya miezi sita kwa sababu sasa biashara inakwenda vizuri ”,anasema.

Hata hivyo anasema katika msimu huu SONAMC imeweza kuingia katika biashara ya mazao ya stakabadhi ghalani katika mazao ya ufuta na soya na kwamba wamefanikiwa kuwaingizia wakulima kupitia NMB shilingi bilioni 16 katika kipindi cha miezi miwili tu kuanzia Mei hadi Julai 2019.

“Zipo Benki nyingi hapa nchini,lakini sisi SONAMC tunafanyakazi na NMB kwa asilimia 95,kwa kifupi NMB ni Benki sikivu,nimesimama hapa kutoa ushuhuda kwamba licha ya kudaiwa na NMB,tusikimbie nenda kawaambie pamoja na kunidai nikopeshe tena tusonge mbele”,anasisitiza.

Naye Meneja wa NMB Tawi la Songea Daniel Zake anawapongeza wafanyabiashara wadogo na wa kati kwa kuunga mkono Benki ya NMB ambapo anaeleza kuwa wafanyabiashara hao ni nguzo muhimu katika Benki hiyo.

Kupitia warsha hiyo wanachama wa NMB Business Club wamechagua viongozi wao wapya ambao wataongoza katika

kipindi kingine cha mwaka mmoja ambapo Mwenyekiti amechaguliwa kuwa ni Michael West,Katibu ni Wilson Nziku na wajumbe watatu ni Hassani Maputo,Happiness Peter na John Mtokambali.

NMB ni miongoni mwa Benki inayoongoza kwa wigo wa huduma za kibenki hapa nchini,ikiwa na matawi 228,mawakala zaidi ya 6,800,mashine za ATM zaidi ya 800 sanjari na kutoahuduma za kibenki kwa njia ya mtandao,ina kituo cha huduma kwa wateja na vituo vya biashara.

**Mwandishi wa makala haya ni Albano Midelo,mawasiliano simu 0784765917,baruapepe: [albano.midelo@gmail.com](mailto:albano.midelo@gmail.com)**